

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WIALAYA YA MVOMERO**

**SHULE YA SEKONDARI MELA**

**S L P**

**MOROGORO**

**KUMB.NO.MSS/J/2020**

**MLEZI/MZAZI WA .....**

**YAH: TAARIFA YA KUCHAGULIWA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021**

1. Ninayo furaha kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga kidato cha KWANZA 2021. Katika shule ya sekondari Mela iliyopo wilaya ya Mvomero, tarafa ya Mlali, katika kata ya Mangae kijiji cha Mela.  
Natumia fursa hii kukupongeza na kukupatia maagizo muhimu ya kujiunga na shule. Muhula wa masomo unaanza tarehe 11/01/2021. Unatakiwa kuripoti shuleni 10/01/2021.  
**NAMNA YA KUFIKA SHULE YA SEKONDARI MELA**  
Shule ya sekondari Mela ipo njia kuu ya kuelekea Iringa . Ipo kilomita 10 kutoka barabara kuu ya Iringa. Ukiwa Morogoro mjini nenda stendi ya daladala ya sabasaba kisha panda gari za kuelekea MELELA au DOMA kisha shuka kituo cha MELELA-KOLOLO. Baada ya hapo tumia usafiri wa pikipiki kufika shule ya sekondari Mela. Nauli ya daladala kutoka mjini Morogoro mpaka kituo cha MELELA – KOLOLO ni Sh. 2,000/= na usafiri wa pikipiki ni kati ya 4,000/= hadi 5,000/=  
**KARIBU SANA MELA SEKONDARI.**

**2.1. MAHITAJI YA LAZIMA YA MWANAFUNZI**

**SARE ZA SHULE**

**A. WAVULANA**

- Masharti meupe mawili (02) yenye mikono mifupi (tomato)
- Suruali yenye marinda na tun-up rangi ya 'DAMU YA MZEE' isiyo ya kubana (02)
- Viatu vyeusi vyenye kamba na visivyo na kisigino kirefu (Jozi mbili).
- Soksi ndefu nyeusi (Jozi mbili).
- T – shirt – inapatikana shuleni.
- Sare yenye rangi ya mitindo na mishono tofauti na taratibu za shule hazitapokelewa
- Suruali ivaliwe na mkanda mweusi usio na kifungio kikubwa au alama au maandishi makubwa.

**B. WASICHANA**

- Masharti meupe mawili (02) yenye mikono mifupi (tomato) na nusu kanzu nyeupe kwa watoto wa kiislamu
- Sketi ya rangi ya 'DAMU YA MZEE' mishono wa rinda box (02) urefu upite magoti TAKRIBANI SENTIMETA 40 kutoka kwenye magoti kushuka chini.
- Viatu vyeusi vyenye kamba na visivyo na kisigino kirefu.
- Hijabu zinaruhusiwa kwa wasichana kufuatana na taratibu za hijabu.

- Hatutapokea sare zisizozingatia maadili.
- Trak suti ya Blue

## 2.0 VIFAA VYA KUJIFUNZIA (MZAZI/MLEZI ANUNUE)

- Madaftari makubwa 09 yenye kurasa 48 au counter book
- Mkebe (mathematical set) moja (01)
- Rula ndefu, kalamu na penseli.
- Begi la kubebea madaftari (mfuko wa Rambo hauruhusiwi kubebea madaftari).

## 3.0 HATI YA LAZIMA

Hati zifuatazo zikamilishwe na kila mwanafunzi aje nazo shuleni kwa ajili ya kumbukumbu zake:

- Nakala ya cheti cha kuzaliwa (01)
- Fomu ya hospitali (Request for Medical Examination). LAZIMA mwanafunzi apimwe na mganga wa serikali na kujaza fomu hiyo kikamilifu.

## 4.0 VIFAA VINGINE

- Godoro dogo futi 3×6 (01)
- Chandarua (01)
- Sahani ya chakula (01)
- Kijiko cha chakula (01)
- Kikombe cha uji (01)
- Bakuli la mboga (01)
- Ndoo ndogo ya lita 10 (02)
- Trunka (01)

## 5.0 HUDUMA YA CHAKULA NA TAHADHARI

Shule ina hosteli kwa ajiri wanafunzi wa kike ambao watakaa humo. Mzazi/Mlezi atalazimika kuchangia huduma ya chakula cha mwanee awapo shuleni. Kutokana na makubaliano na wazazi/walezi KILA MZAZI/MLEZI ATACHANGIA JUMLA YA SHILINGI LAKI NNE ( 400,000) KWA MWAKA

Fedha hizi zinatakiwa zilipwe kwa awamu mbili au mara moja kwa mkupuo (200,000/= awamu ya kwanza na Tsh 200,000/= awamu ya pili )

Pesa ya tahadhari Tsh 10,000/=

## 6.0 MUHIMU

Siku ya kuripoti shuleni ni tarehe 10.1.2021 lazima mzazi/mlezi amlete mtoto wake. Fika moja kwa moja ofisi ya mkuu wa shule/Makamu mkuu wa shule ili kumuandikisha mtoto.

## MWISHO

Ni matumaini yetu kuwa kila mwanafunzi na mzazi/ mlezi atafuata na kuzingatia mambo yote yaliyoorodheshwa hapo juu kwa lengo la kufanikishwa malezi na utoaji wa elimu bora hapa Mela Sekondari.

KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI MELA

*S.J. Mwafuma*  
MKUU WA SHULE  
0628481573

MAKAMU MKUU WA SHULE  
0764-600097

